TANGAZO LA SERIKALI Na. 225 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA KUZUIA NA KUDHIBITI SUMUKUVU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 263 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Kuzuia na Kudhibiti Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Kuzuia na Kudhibiti Sumukuvu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama “Sheria Ndogo kuu”.

Marekebisho ya kanuni ya 3

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kuongeza tafsiri ya msamiati ufuatao kwa kuzingatia mtiririko wa kialfabeti:

“kalenda ya kilimo” maana yake ni mtiririko wa shughuli za kilimo kwa msimu husika kuanzia mwanzo wa msimu hadi mwisho wa msimu;”.

Marekebisho ya kanuni ya 13

**3**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 13-

(a) kwa kupangilia upya masharti ya kanuni hiyo kuwa kanuni ndogo ya (1);
(b) kwa kuondoa maneno “vifungashio na” yaliyopo katika kanuni ndogo ya (1) iliyopangiliwa upya; na
(c) kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (1) iliyopangiliwa upya kanuni ndogo mpya ifuatayo:

"(2) Mmiliki wa mazao anayesafirisha mazao yake anapaswa kuhakikisha vifungashio na vifaa anavyotumia kusafirisha mazao ni vikavu au visivyoruhusu maji au unyevu na vumbi kuingia ndani ili kuepusha kuvu kuota kwenye mazao.".

Marekebisho ya kanuni ya 16

**4**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 16 kwa-

(a) kuongeza maneno "bila kuwa na sababu ya msingi" mwanzoni mwa aya za (a), (b) na (c); na

(b) kufuta neno "hataanika" lililopo mwanzoni mwa aya (d) na badala yake kuweka maneno "ataanika mazao".

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*